



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
NAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO
YA UFUNDI STADI



MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 10 mwezi 02 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MARA UTC, S.L.P. 188,
MUSOMA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya
Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama
"Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

JUMA N. MWANZI S.L.P. 194, MUSOMA
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
BUTHAMA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali
za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
BUTHAMA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya
KUWEKA UGAE KATIKA BWENI LA WASICHANA

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na
Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi
itakavyofanyika;

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA VETA-
MARA.

Jina: DAVID LOUIS Saini: _____




VTC MANAGER
D. MARA VTC
P. O. BOX 188
MUSOMA

Wadhifa: Msimamizi wa Maadi
BUTAMA DVCC Tarehe: 10/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G KIDIRI Saini: _____



Wadhifa: AFISA MANENUZI Tarehe: 10/02/2022

REGISTRATION OFFICER
MARA VTC
P. O. BOX 188
MUSOMA - MARA

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: JUMA N. MWAZI Mbele ya _____
Saini: Juma N. Mwaizi

Wadhifa: FUNDI Tarehe: 10.2.22

Mbele ya (Shahidi)

Jina: SAMBI MJIUHU Saini: MJIUHU

Wadhifa: FUNDI shahidi Tarehe: 10-02-2022

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 1,800,000.00, Fundi atafanya kazi ya KUWEKA VIGAE kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapo kuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80: 30% ya Gharama ya Ufundi;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi; na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio": 5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 15 mwezi 03 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 35 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

- (a) Kujenga KUWEKA VIGAE na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;